102/3
**KISWAHILI**
Karatasi 3
Julai/Agosti 2016
**Muda: Saa 2½**

# NTIMA, NYAKI AND MUNICIPALITY CLUSTER EVALUATION 2016

**KISWAHILI**
Karatasi 3
Julai/Agosti 2016
**Muda: Saa 2½**

## MAAGIZO

* Jibu maswali **manne** pekee.
* Swali la kwanza ni la **lazima**.
* Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Riwaya,Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi
* Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
* Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
* Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

## SEHEMU A : USHAIRI

**1. LAZIMA**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Naingia ukumbini, nyote kuwakariria,
Ushairi niwapeni, hoja nitawaachia,
Mnipe masikioni, shike nachoelezea,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Naanza kwa uzalendo, nchi yetu tuipende,
Yadhihirishe matendo, nchi yetu tuilinde,
Wa kila mtu mwendo, usije kawa mpinde,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili

Wote tuwe na umoja, tuuache ukabila
Kabila lisiwe hoja, mwenza kumnyima hela,
Taifa letu ni moja, Mkenya ndilo kabila,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Linda demokrasia, uongozi tushiriki,
Haki kujielezea, wachotaka na hutaki,
Changu naweza tetea, demokrasia haki,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tena adili usawa, mgao raslimali,
Bajeti inapogawa, isawazishe ratili,
Idara zilizoundwa, ‘faidi kila mahali,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tuwe na uadilifu, twache tamaa ya hongo,
Tusiwe na udhaifu, wa kuwa watu waongo,
Tukomeshe uhalifu, kisha tuache maringo,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Ubinafsi si adili, ila ni kusaidia,
Ukiwa nayo mali, asiyenacho patia,
Kama mtu mswahili, ubinafsi achia,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Na inavyoelezea, katiba ni kielezi,
Tutii kwa mazoea, hadi kijacho kizazi,
Kwa hayo nitamwachia, hiyo ya ziada kazi,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili

**a)** Eleza mambo yoyote **manne** ambayo mshairi anashauri taifa lifanye ili kuwa na maadili. (alama 4)

**b)** Taja tamathali yoyote **moja** inayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)

**c)** Ainisha shairi hili kwa kuzingatia kigezo kifuatacho : (alama 1)
Mpangilio wa vina

**d)** Bainisha nafsineni (mzungumzaji) katika shairi hili. (alama 2)
**e)** Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

**f)** Eleza umuhimu wa aina **mbili** za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa nne. (alama 4)

**g)** Andika ubeti wa **pili** kwa lugha nathari. (alama 4)

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

**h)** Eleza maana ya neno lifuatalo kama lilivyotumiwa katika shairi :
i) hongo (alama 1)

## SEHEMU B : RIWAYA
**K.Walibora : Kidagaa Kimemwozea**
**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** "Lakini bila matumaini hatuwezi kwenda mbele na Revolution."
**a)** i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii) Bainisha tamathali **moja** ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

**b)** Kwa kufafanua hoja saba thibitisha kwamba kuna haja ya kuwa na Revolution. (alama 14)

**3.** Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)
a) Sadfa
b) Taharuki

## SEHEMU C : TAMTHILIA
**T.M. Arege : Mstahiki Meya**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Tayari nimemkabidhi barua ya kujiuzulu anayehusika."
**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
**b)** Mbali na changamoto inayofanya msemaji kujiuzulu, jadili changamoto nyinginezo zinazowakumba wanacheneo. (alama 16)

**5.** "Lazima kwanza mnihakikishie kuwa huyo sumu hapati hata fununu ya jambo hili."
**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

**b)** Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (alama 8)

**c)** Andika umuhimu wa huyo sumu. (alama 8)

## SEHEMU D : HADITHI FUPI
**K. Walibora na S.A. Mohammed (Wah): Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**
**Jibu swali la 6 au la 7**

**"Mwana wa Darubini (K.Mwende Mbai)**

**6.** "Uniulie nini na ndoa yetu na wewe inamhusu pia yeye?"
**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

**b)** Eleza sifa zozote nne za msemewa. (alama 8)

**c)** Jadili madhila yanayomkumba mwanamke katika hadithi hii. (alama 8)

**7. "Tazamana na Mauti" (S.A. Mohammed)**

Tamaa mbele mauti nyuma. Thibitisha ukweli ya methali hii ukirejelea hadithi ya Tazamana na mauti. (alama 20)

## SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI
**Jibu swali la 8**

**8. a)** Eleza kikamilifu nafasi / umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii ya kisasa. (alama 5)

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

**b)** Jadili matatizo matano yanayomkabili mkusanyaji / mtafiti wa data ya fasihi simulizi. (alama 5)

**c)** Eleza maana ya istilahi zifuatazo za fasihi simulizi. (alama 10)

i) Rara nafsi
ii) Hotuba
iii) Miviga
iv) Ulumbi
v) Ngomezi

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479